WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
TAASISI YA ELIMU TANZANIA

MUHTASARI WA SOMO LA STADI ZA MAWASILIANO KWA MWALIMU TARAJALI WA FANI YA UZIWI ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU MAALUMU

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019

ISBN: 978-9976-61-837-2

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam
Tanzania

Simu: +255 222 773 005
Faksi: +255 222 774 420
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). Muhtasari wa somo la Stadi za Mawasiliano kwa Mwalimu Tarajali Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kuutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

Idhini

Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kumuandaa mwalimu tarajali kuwa mahiri na mwenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati na kwa weledi. Mwalimu huyo atafundisha katika shule za msingi zinazodahili wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Mwalimu tarajali atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhitimu mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu na kufaulu mafunzo ya nadharia na mafunzo ya ualimu kwa vitendo.

Muhtasari huu umeidhinishwa kuwa ni wa somo la Stadi za Mawasiliano katika Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kaimu Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
S.L.P. 10
Dodoma
Simu: +255 262 963 533
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

YALIYOMO

Idhini iii

1.0 Taarifa za Awali 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Muundo wa Muhtasari 1

1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari 2

1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania 2

1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu 3

1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu 4

1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu 4

1.8 Malengo ya Somo la Stadi za Mawasiliano 5

1.9 Upimaji na Tathmini 5

1.10 Muda wa Mafunzo 6

1.11 Maudhui ya Muhtasari wa Somo 7

2.0 Maudhui ya Muhtasari 8

2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo 8

2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo 10

Majedwali

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati 6

Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Stadi za Mawasiliano kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Uziwi ... 8

Jedwali namba 3: Maudhui ya Ufundishaji wa Somo la Stadi za Mawasiliano kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Uziwi 10

Orodha ya Machapisho 28

1.0 TAARIFA ZA AWALI

1.1 Utangulizi

Muhtasari huu wa somo la Stadi za Mawasiliano umeandaliwa kutokana na Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu wa mwaka 2019. Muhtasari huu unalenga kumjengea mwalimu tarajali maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kukabiliana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi kiziwi aliyedahiliwa katika elimu ya msingi.

Ili kumsaidia mkufunzi, yametolewa mapendekezo ya mbinu za kufundishia na kujifunzia, zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na upimaji. Mkufunzi anahimizwa kutumia mbinu mbalimbali na zana zinazopatikana kwenye mazingira yanayohusika na upimaji ulioshauriwa kwenye muhtasari huu. Pamoja na mbinu zilizoainishwa kwenye muhtasari huu mkufunzi anaweza kutumia mbinu nyingine tofautitofauti kulingana na mazingira na mahitaji ya mwalimu tarajali na umahiri unaojengwa.

1.2 Muundo wa Muhtasari

Muhtasari huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ina taarifa za awali na sehemu ya pili ni maudhui ya muhtasari.

Sehemu ya kwanza inajumuisha utangulizi, muundo wa muhtasari, sababu za kuandaa muhtasari, malengo ya elimu nchini Tanzania, malengo ya jumla ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, madhumuni ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, umahiri wa jumla wa mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, malengo ya somo la Stadi za Mawasiliano, upimaji na tathmini na muda wa mafunzo. Sehemu ya pili inajumuisha maudhui ya muhtasari wa somo.

1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari

Dira ya elimu na mafunzo inasisitiza kuwapo kwa mwalimu aliye bora kitaaluma na kitaalamu na mwenye mbinu mbalimbali za kujifunzia na kufundishia somo la Stadi za Mawasiliano ili kukabiliana na changamoto za mahitaji na matarajio ya kielimu kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mwelekeo wa dira na mpango wa elimu kwa ujumla ni kumwandaa mwalimu mwenye ujuzi wa kumfundisha mwanafunzi kiziwi katika shule za msingi kwa kuzingatia misingi, kanuni na mielekeo inayopasa. Mwalimu tarajali wa somo la Stadi za Mawasiliano kwa ajili ya mwanafunzi kiziwi anahitaji kupata ujuzi wa kuweza kuyatumia vema mazingira yake.

1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania

Elimu inayotolewa ni ya kurithisha maarifa, stadi na mielekeo bora kutoka kwa vizazi vilivyopita hadi vizazi vya wakati huu na vijavyo. Hivyo, yafuatayo ndiyo malengo makuu ya elimu nchini:

a) kuendeleza na kukuza maendeleo, kuboresha haiba ya wananchi wa Tanzania, rasilimali zao na matumizi bora ya rasilimali hizo katika kuleta maendeleo ya mtu binafsi na ya kitaifa;
b) kukuza tabia ya kuthamini utamaduni, mila na desturi za watanzania;
c) kukuza upatikanaji wa fursa za kusoma, kuandika na kuhesabu na matumizi sahihi ya maarifa na stadi za kijamii, kisayansi, kiufundi, kiteknolojia, kitaalamu na aina nyingine za maarifa na ujuzi, kwa ajili ya maendeleo na kuboresha hali ya mtu na jamii;
d) kukuza na kuendeleza kujiamini, kudadisi, weledi na kuheshimu utu wa mtu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza na kwa maendeleo ya Taifa;
e) kuwezesha na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, kuboresha na kukuza stadi za kiakili, utendaji, uzalishaji na nyingine zinazotakiwa katika kukidhi mabadiliko ya mahitaji kiuchumi;

f) kumwezesha kila raia kuelewa misingi ya katiba ya nchi pamoja na kuthamini haki za binadamu na uraia, wajibu na majukumu yanayoendana nayo;
g) kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi za kujiajiri na kuajiriwa na kuboresha utendaji kazi katika sekta za uzalishaji na huduma;
h) kujenga misingi ya maadili yanayokubalika kitaifa na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na sheria kwa njia ya kujifunza;
i) kuwezesha kuwapo kwa matumizi sahihi, usimamizi na utunzaji wa mazingira; na
j) kujenga tabia na utamaduni wa kuwakubali watu wenye ulemavu na kuwashirikisha kwenye nyanja zote za maisha kwa maendeleo ya Taifa.

1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu yana malengo yafuatayo:

a) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika nadharia za saikolojia ya elimu, malezi, ushauri na huduma kwa watu wenye ulemavu;
b) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kugundua na kubuni mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia;
c) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika uchambuzi wa mtaala na vifaa vya mtaala;
d) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kumudu stadi kuu za masomo ya lugha, sanaa na maendeleo ya sayansi na teknolojia;
e) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kufanya upimaji na tathmini ya maendeleo katika elimu;
f) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika stadi za uongozi na utawala katika elimu; na
g) kujenga umahiri wa mwalimu tarajali katika kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.

1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mwishoni mwa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ya miaka miwili, mwalimu tarajali aweze:

a) kutafsiri mtaala wa elimu ya msingi na mihtasari yake katika masomo darasani;
b) kuandaa na kutumia njia shirikishi katika ufundishaji/ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
c) kubuni, kuendeleza na kufaragua zana za ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
d) kufanya tafiti tatuzi za kielimu ili kuwabaini, kuwaendeleza na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
e) kurithisha desturi, maadili na tabia zinazokubalika kwa wanafunzi wa shule za msingi;
f) kuchagua, kupanga, kusimamia na kuongoza vipindi darasani katika shule za msingi;
g) kufundisha kwa ufanisi masuala mtambuka; na
h) kutunga na kusahihisha majaribio na mitihani inayoendana na mtaala wa elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi katika nyanja zote tatu za kujifunza.

1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Umahiri mkuu wa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umejikita katika kumwandaa mwalimu tarajali aweze:

a) kumbaini mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu, kujenga misingi ya kukubalika kwa wenzake, kwa jamii na kumpatia afua stahiki;
b) kutumia mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu;
c) kutumia njia mbalimbali za mawasiliano na teknolojia saidizi kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya mwanafunzi;
d) kutumia mbinu mbalimbali katika kutambua vipaji walivyonavyo wanafunzi wenye mahitaji maalumu na namna ya kuviendeleza;

e) kufanya tafiti tatuzi za kielimu kwa wanafunzi ili kuwabaini na kuwasaidia wale wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
f) kutumia misingi na stadi za uongozi katika kuongoza taasisi mbalimbali za elimu;
g) kutumia, kutunza na kukarabati vifaa saidizi vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
h) kutumia sanaa na michezo rekebifu katika kuibua na kuendeleza vipaji mbalimbali vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
i) kutumia misingi ya ufundishaji na ujifunzaji kufundishia masomo ya taaluma;
j) kujenga umahiri wa masomo kwa mwalimu tarajali utakaomwezesha kuelewa masomo vema na hivyo kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu; na
k) kushirikiana na familia za wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kuwajengea wanafunzi hao kujiamini, tabia ya kujifunza na kukuza vipaji walivyonavyo.

1.8 Malengo ya Somo la Stadi za Mawasiliano

Malengo ya Muhtasari wa Stadi za Mawasiliano ni kumwandaa mwalimu tarajali wa fani ya uziwi kuweza:

a) kutumia stadi za mawasiliano kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi;
b) kutumia stadi za mawasiliano na Lugha ya Alama katika ufundishaji na ujifunzaji; na
c) kubaini njia za mawasiliano katika ufundishaji na ujifunzaji.

1.9 Upimaji na Tathmini

Muhtasari huu umependekeza mbinu mbalimbali za upimaji na tathmini kwa kuzingatia mahitaji ya mwalimu tarajali wakati wa mchakato wa ujifunzaji wa kozi ya ualimu. Upimaji tamati utafanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania na utakuwa na alama 50. Upimaji endelevu utafanywa na mkufunzi wakati mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unaendelea na utakuwa na alama 50.

Upimaji huu unahusisha majaribio, kazimradi, kazi binafsi, mkoba wa kazi, kazi kwa vitendo na mtihani wa mwisho wa muhula. Uzito wa kila aina ya upimaji umeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati

Vipengele	**Njia za Upimaji**	**Mwaka**				**Idadi**	**Alama (%)**
		Mwaka wa I		**Mwaka wa II**			
		Muhula wa I	**Muhula wa II**	**Muhula wa I**	**Muhula wa II**		
Taaluma	Majaribio	1	1	1	1	4	10
	Kazimradi	1	-	1	-	2	5
	Kazi binafsi	1	1	1	-	3	5
	Kazi kwa vitendo	1	1	1	-	3	5
	Mkoba wa kazi	1	-	1	-	2	5
	Mtihani wa mwisho wa muhula	1	1	1		3	20
Upimaji endelevu							50
Upimaji tamati: Mtihani wa Baraza la Mitihani la Tanzania.					1	1	50
Jumla ya alama za upimaji endelevu na upimaji tamati							**100**

1.10 Muda wa Mafunzo

Muhtasari huu wa somo la Stadi za Mawasiliano kwa fani ya uziwi umekusudiwa kukamilishwa kwa kipindi cha miaka miwili. Mtazamo wa somo hili ni kumjengea mwalimu tarajali misingi muhimu ya maarifa ya somo la Stadi za Mawasiliano itakayomwezesha kumfundisha kikamilifu mwanafunzi kiziwi kumudu ujifunzaji katika elimu ya msingi

1.11 Maudhui ya Muhtasari wa Somo

Maudhui ya muhtasari yamepangwa katika jedwali yakihusisha umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali, vigezo vya upimaji, viwango vya utendaji na idadi ya vipindi

1.11.1 Umahiri

Ni uwezo wa kufikiri na kutenda kwa ufanisi

1.11.2 Umahiri Mkuu

Ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na ufanisi unaokusudiwa kufikiwa na mwalimu tarajali baada ya kujifunza kwa muda fulani. Hujengwa na umahiri mahususi kadhaa atakaoujenga mwalimu tarajali kwa kutenda shughuli mbalimbali

1.11.3 Umahiri Mahususi

Ni uwezo atakaojengewa mwalimu tarajali katika kutenda shughuli mbalimbali kwa muda maalumu

1.11.4 Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali

Ni vitendo ambavyo mwalimu tarajali anapaswa kuvifanya ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa

1.11.5 Vigezo vya Upimaji

Ni viwango vya ufanisi wa utendaji wa mwalimu tarajali ili kufikia umahiri mahususi

1.11.6 Viwango vya Utendaji

Ni kiasi cha ufikiwaji wa vigezo vya kila shughuli anayotenda mwalimu tarajali

1.11.7 Idadi ya Vipindi

Idadi ya vipindi ni makadirio ya muda utakaotumika katika kufundisha na kujifunza kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Somo hili litafundishwa kwa vipindi viwili (2) kwa wiki. Hata hivyo mapendekezo haya ya idadi ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

2.0 MAUDHUI YA MUHTASARI

2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo

Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Stadi za Mawasiliano kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Uziwi

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1. Kutumia stadi za mawasiliano kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi	1.1 Kuchambua mbinu za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi 1.2 Kueleza njia mbadala za mawasiliano 1.3 Kujenga uwezo wa kutumia teknolojia saidizi katika kukuza stadi za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi 1.4 Kutumia njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi
2. Kutumia stadi za ukalimani wa Lugha ya Alama kumuwezesha mwanafunzi kiziwi kuwasiliana	2.1 Kuchambua lugha ya alama 2.2 Kukalimani lugha ya mazungumzo kwa LAT 2.3 Kukuza stadi za ukalimani wa LAT katika mawasiliano

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
3. Kutumia stadi za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	3.1 Kubaini njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi 3.2 Kutumia njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi 3.3 Kutumia TEHAMA katika mawasiliano kwa ufundishaji na ujifunzaji kwa mwanafunzi kiziwi
4. Kutumia mbinu mbalimbali kuwezesha ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa kumuwezesha mwanafunzi kiziwi kuwasiliana	4.1 Kujenga uwezo wa kufundisha stadi ya kusoma 4.2 Kutumia mbinu mbalimbali za kumuwezesha mwalimu tarajali kufundisha kuandika 4.3 Kujenga uwezo wa kuchakata mbinu mbalimbali za kufundishia stadi ya kuhesabu

2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo

Jedwali namba 3: Maudhui ya Ufundishaji wa Somo la Stadi za Mawasiliano kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Uziwi

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
1.0 Kutumia stadi za mawasiliano kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi	1.1 Kuchambua mbinu za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	a) Kufafanua dhana ya mawasiliano	Dhana ya mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi imefafanuliwa.	Anafafanua dhana ya mawasiliano kwa kuzingatia maana.	Anafafanua dhana ya mawasiliano kwa kuzingatia maana na aina.	Anafafanua dhana ya mawasiliano kwa mwanafunzi kwa kuzingatia maana, aina na umuhimu.	Anafafanua dhana ya mawasiliano kwa mwanafunzi kwa kuzingatia maana, aina na umuhimu na kwa kutoa mifano kulingana na muktadha.	8
		b) Kubainisha mbinu za mawasiliano	Mbinu sita za mawasiliano zimebainishwa.	Anabainisha mbinu tatu za mawasiliano.	Anabainisha mbinu nne za mawasiliano.	Anabainisha mbinu tano za mawasiliano.	Anabainisha mbinu sita za mawasiliano na kutoa mifano kwa kuzingatia muktadha.	
		c) Kuainisha changamoto za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	Changamoto za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi zimeainishwa.	Anaainisha changamoto za mawasiliano za darasani kwa mwanafunzi.	Anaainisha changamoto za mawasiliano za darasani na nje ya darasa kwa mwanafunzi.	Anaainisha na kuelezea changamoto za mawasiliano za darasani, nje ya darasa kwa mwanafunzi.	Anaainisha na kuelezea changamoto za mawasiliano za darasani, nje ya darasa na kwenye jamii kwa mwanafunzi na kutoa mifano.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		d) Kubaini mbinu za mawasiliano zinazotumika darasani	Mbinu tano za mawasiliano katika ufundishaji na ujifunzaji zimebainishwa.	Anabainisha mbinu moja ya ufundishaji na ujifunzaji.	Anabainisha mbinu tatu za ufundishaji na ujifunzaji.	Anabainisha mbinu nne za ufundishaji na ujifunzaji.	Anabainisha mbinu tano za ufundishaji na ujifunzaji na kutoa mifano kwa kuhusianisha na mazingira yanayomzunguka.	
	1.2 Kueleza njia mbadala za mawasiliano	a) Kufafanua dhana ya njia mbadala za mawasiliano	Dhana ya njia mbadala za mawasiliano zimefafanuliwa.	Anafafanua dhana ya njia mbadala za mawasiliano kwa kuzingatia maana.	Anafafanua dhana ya njia mbadala za mawasiliano kwa kuzingatia maana na aina.	Anafafanua dhana ya njia mbadala za mawasiliano kwa kuzingatia maana, aina na umuhimu.	Anafafanua dhana ya njia mbadala za mawasiliano kwa kuzingatia maana, aina, umuhimu na kutoa mifano kwa kuzingatia muktadha.	8
		b) Kubainisha njia mbadala za mawasiliano	Njia tatu mbadala za mawasiliano zimebainishwa.	Anabainisha njia moja mbadala ya mawasiliano.	Anabainisha njia mbili mbadala za mawasiliano.	Anabainisha njia tatu mbadala za mawasiliano.	Anabainisha njia tatu mbadala za mawasiliano na kutoa mifano kwa kuzingatia muktadha.	
		c) Kueleza njia za mawasiliano	Njia tatu za mawasiliano zimeelezwa.	Anaeleza njia moja ya mawasiliano.	Anaeleza njia mbili za mawasiliano.	Anaeleza njia tatu za mawasiliano.	Anaeleza njia tatu za mawasiliano na kutoa mifano kwa kuzingatia muktadha.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		d) Kutumia njia mbadala za mawasiliano	Njia tatu mbadala za mawasiliano zimetumika.	Anatumia njia moja mbadala ya mawasiliano.	Anatumia njia mbili mbadala za mawasiliano.	Anatumia njia tatu mbadala za mawasiliano.	Anatumia njia tatu mbadala za mawasiliano kwa mifano na kuzingatia mazingira halisi.	
	1.3 Kujenga uwezo wa kutumia teknolojia saidizi katika kukuza stadi za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	a) Kufafanua dhana ya teknolojia saidizi katika mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	Dhana ya teknolojia saidizi katika mawasiliano imefafanuliwa.	Anafafanua dhana ya teknolojia saidizi katika mawasiliano kwa kuzingatia maana.	Anafafanua dhana ya teknolojia saidizi katika mawasiliano kwa kuzingatia maana na sifa.	Anafafanua dhana ya teknolojia saidizi katika mawasiliano kwa kuzingatia maana, sifa na umuhimu.	Anafafanua dhana ya teknolojia saidizi katika mawasiliano kuzingatia maana, sifa, umuhimu na kutoa mifano kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi.	9
		b) Kujadili mambo ya kuzingatia katika kutumia teknolojia saidizi katika kukuza stadi za mawasiliano	Mambo ya kuzingatia katika kutumia teknolojia saidizi katika kukuza stadi za mawasiliano, mfano usalama, ukarabati na uhifadhi yamejadiliwa.	Anajadili usalama katika kutumia teknolojia saidizi katika kukuza stadi za mawasiliano.	Anajadili usalama na ukarabati katika kutumia teknolojia saidizi kukuza stadi za mawasiliano.	Anajadili usalama, ukarabati na uhifadhi katika kutumia teknolojia saidizi kukuza stadi za mawasiliano.	Anajadili usalama, ukarabati na uhifadhi katika kutumia teknolojia saidizi kukuza stadi za mawasiliano na kutoa mifano kulingana na mazingira yake.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kubainisha vifaa stahiki vya teknolojia saidizi katika mawasiliano	Vifaa stahiki vitano vya teknolojia saidizi katika mawasiliano vimebainishwa.	Anabainisha kifaa stahiki kimoja cha teknolojia saidizi katika mawasiliano.	Anabainisha vifaa stahiki viwili vya teknolojia saidizi katika mawasiliano.	Anabainisha vifaa stahiki vitatu vya teknolojia saidizi katika mawasiliano.	Anabainisha vifaa stahiki vitano vya teknolojia saidizi katika mawasiliano na kuzingatia vilivyopo katika mazingira.	
		d) Kutumia vifaa stahiki vya teknolojia saidizi katika mawasiliano ya mwanafunzi kiziwi	Vifaa stahiki vitano katika teknolojia saidizi katika mawasiliano vimetumika.	Anatumia kifaa stahiki kimoja cha teknolojia saidizi katika mawasiliano.	Anatumia vifaa stahiki viwili vya teknolojia saidizi katika mawasiliano.	Anatumia vifaa stahiki vitatu vya teknolojia saidizi katika mawasiliano.	Anatumia vifaa stahiki vitano vya teknolojia saidizi katika mawasiliano na kuzingatia mazingira yake.	
		e) Kufafanua dhana ya mawasiliano kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi kiziwi	Dhana ya mawasiliano kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi kiziwi (maana, aina, umuhimu na vikwazo vya mawasiliano) imefafanuliwa.	Anafafanua maana ya mawasiliano.	Anafafanua maana na aina za mawasiliano.	Anafafanua maana, aina na umuhimu wa mawasiliano.	Anafafanua maana, aina, umuhimu na vikwazo vya mawasiliano.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	1.4 Kutumia njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	a) Kubaini vigezo vya kuzingatia wakati wa kuchagua njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	Vigezo vitano vya kuzingatia wakati wa kuchagua njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi vimebainishwa.	Anabainisha kigezo kimoja cha kuchagua njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi.	Anabainisha vigezo viwili vya kuchagua njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi.	Anabainisha vigezo vitatu vya kuchagua njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi na kutoa mifano.	Anabainisha vigezo vitano vya kuchagua njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi na kutoa mifano kwa kuhusianisha na mazingira.	8
		b) Kufafanua vijenzi vya mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	Vijenzi vitano vya mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi vimefafanuliwa.	Anafafanua vijenzi viwili vya mawasiliano.	Anafafanua vijenzi vitatu vya mawasiliano.	Anafafanua vijenzi vinne vya mawasiliano.	Anafafanua vijenzi vitano vya mawasiliano na kutoa mifano.	
		c) Kufafanua mbinu za mawasiliano	Mbinu tano za mawasiliano zimefafanuliwa.	Anafafanua mbinu moja ya mawasiliano.	Anafafanua mbinu mbili za mawasiliano na kuelezea faida na hasara zake.	Anafafanua mbinu tatu za mawasiliano na kuelezea faida na hasara zake.	Anafafanua mbinu tano za mawasiliano na kuelezea faida na hasara zake na kutoa mifano kwa kuzingatia mazingira halisi.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		d) Kufafanua mbinu za masikivu-maongezi katika mawasiliano	Mbinu tano za masikivu-maongezi zimefafanuliwa.	Anafafanua mbinu moja ya masikivu-maongezi.	Anafafanua mbinu mbili za masikivu-maongezi.	Anafafanua mbinu tatu za masikivu-maongezi na kutoa mifano.	Anafafanua mbinu tano za masikivu-maongezi na kutoa mifano kwa kuzingatia mazingira halisi.	
2.0 Kutumia stadi za ukalimani wa Lugha ya alama kumuwezesha mwanafunzi kiziwi kuwasiliana	2.1 Kuchambua lugha ya alama	a) Kufafanua dhana ya lugha ya alama	Dhana ya lugha ya alama imefafanuliwa.	Anafafanua maana ya lugha ya alama.	Anafafanua maana na aina ya lugha ya alama.	Anafafanua maana, aina na umuhimu wa lugha ya alama.	Anafafanua maana, aina, umuhimu wa lugha ya alama na kuitofautisha na lugha nyingine na kutoa mifano.	7
		b) Kueleza maendeleo ya LAT katika mawasiliano	Maendeleo ya LAT katika mawasiliano yameelezwa.	Anaeleza historia na kukubalika kwa LAT kama lugha.	Anaeleza historia na kukubalika kwa LAT kama lugha na usanifishaji wake.	Anaeleza historia na kukubalika kwa LAT kama lugha, usanifishaji na utunzi wa kamusi.	Anaeleza historia na kukubalika kwa LAT kama lugha, usanifishaji, utunzi wa kamusi na matumizi ya LAT kama lugha ya kufundishia shuleni.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kubainisha utamaduni wa viziwi	Utamaduni wa viziwi umebainishwa.	Anabainisha uhusiano wa LAT na utamaduni wa viziwi.	Anabainisha na kueleza umuhimu na uhusiano wa LAT katika utamaduni wa vikundi vya viziwi.	Anabainisha na kueleza uhusiano na umuhimu wa LAT katika utamaduni, vikundi, na kubadilishana taarifa miongoni mwa viziwi.	Anabainisha na kueleza uhusiano na umuhimu wa LAT katika utamaduni, vikundi, kubadilishana taarifa miongoni mwa viziwi na kutoa mifano.	
	2.2 Kukalimani Lugha ya mazungumzo kwa LAT	a) Kueleza dhana ya ukalimani wa lugha ya alama	Dhana ya ukalimani wa lugha ya alama imeelezwa.	Anaeleza maana ya ukalimani wa lugha ya alama.	Anaeleza maana na aina ya ukalimani wa lugha ya alama.	Anaeleza maana, aina na umuhimu wa ukalimani wa lugha ya alama.	Anaeleza maana, aina na umuhimu wa ukalimani wa lugha ya alama na kutoa mifano.	8
		b) Kubainisha sifa za mkalimani	Sifa tano za mkalimani zimebainishwa.	Anabainisha sifa moja ya mkalimani katika ufahamu wa lugha.	Anabainisha sifa mbili za mkalimani katika ufahamu wa lugha na utamaduni wa jamii ya viziwi na jamii ya wanaosikia.	Anabainisha sifa tatu za mkalimani katika ufahamu wa lugha na utamaduni wa jamii ya viziwi na jamii ya wanaosikia na kutoa mifano.	Anabainisha sifa tano za mkalimani katika ufahamu wa lugha, utamaduni wa jamii ya viziwi na jamii ya wanaosikia na upana wa maarifa katika ukalimani na kutoa mifano.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kuelezea maadili ya ukalimani	Maadili ya ukalimani yameelezewa.	Anaelezea maana ya maadili ya ukalimani.	Anataja na anaelezea maadili ya ukalimani.	Anataja, anaelezea na kufafanua umuhimu wa maadili ya ukalimani.	Anataja, anaelezea na anafafanua umuhimu wa maadili ya ukalimani kwa kuhusianisha na maadili mengine.	
		d) Kubainisha mbinu za ukalimani	Mbinu za awali na mbinu kuu za ukalimani zimebainishwa.	Anabainisha mbinu za awali za kukalimani.	Anabainisha mbinu za awali na mbinu kuu za kukalimani.	Anabainisha mbinu za awali na mbinu kuu za kukalimani kulingana na muktadha.	Anabainisha mbinu za awali na mbinu kuu za kukalimani kulingana na muktadha na kuhusianisha na mazingira.	
	2.3 Kukuza stadi za ukalimani wa LAT katika mawasiliano	a) Kufanya ukalimani wa LAT katika mazingira ya maisha ya kawaida	Ukalimani katika mazingira ya maisha ya kawaida umefanyika.	Anafanya ukalimani wa tungo fupi sahili katika mazungumzo ya kawaida.	Anafanya ukalimani wa tungo fupi zenye sentensi ambatano katika mazungumzo ya kawaida.	Anafanya ukalimani wa tungo fupi zenye sentensi ambatano na changamano katika mazungumzo ya kawaida.	Anafanya ukalimani wa tungo fupi na tungo ndefu zenye sentensi ambatano na changamano katika mazungumzo ya kawaida.	10

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kufanya ukalimani wa LAT katika masomo ya Sayansi na Teknolojia, Hisabati na TEHAMA	Ukalimani wa LAT katika masomo ya Sayansi na Teknolojia, Hisabati na TEHAMA umefanyika.	Anafanya ukalimani katika somo la Hisabati.	Anafanya ukalimani katika masomo ya Sayansi na Teknolojia na Hisabati.	Anafanya ukalimani katika masomo ya Sayansi na Teknolojia, Hisabati na TEHAMA.	Anafanya ukalimani katika masomo ya Sayansi na Teknolojia, Hisabati na TEHAMA na kutofautisha namna ya kukalimani katika masomo hayo.	
		c) Kufanya ukalimani wa LAT katika masomo ya lugha na Maarifa ya Jamii	Ukalimani wa LAT katika masomo ya lugha na Maarifa ya Jamii umefanyika.	Anafanya ukalimani katika somo la Kiswahili.	Anafanya ukalimani katika masomo ya Kiswahili na Kiingereza.	Anafanya ukalimani katika masomo ya Kiswahili, Kiingereza na Maarifa ya Jamii.	Anafanya ukalimani katika masomo ya lugha na Maarifa ya Jamii na kutoa mifano halisi.	
		d) Kufanya ukalimani wa LAT katika masomo ya sanaa, michezo na Stadi za Kazi	Ukalimani wa LAT katika masomo ya sanaa, michezo na Stadi za Kazi umefanyika.	Anafanya ukalimani katika somo la sanaa.	Anafanya ukalimani katika masomo ya sanaa na michezo miwili.	Anafanya ukalimani katika masomo ya sanaa na michezo minne.	Anafanya ukalimani katika masomo ya sanaa, michezo mbalimbali na Stadi za Kazi.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		e) Kufanya ukalimani wa LAT katika masomo ya Uraia na Maadili na Dini	Ukalimani wa LAT katika masomo ya Uraia na Maadili na Dini umefanyika.	Anafanya ukalimani katika masomo ya Uraia na Maadili.	Anafanya ukalimani katika masomo ya Uraia na Maadili na kutoa mifano.	Anafanya ukalimani katika masomo ya Uraia na Maadili na Dini na kutoa mifano.	Anafanya ukalimani katika masomo ya Uraia na Maadili na Dini kwa kuhusianisha mazingira halisi.	
3.0 Kutumia stadi za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	3.1 Kubaini njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	a) Kufafanua dhana ya mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	Dhana ya mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi imefafanuliwa.	Anafafanua maana ya mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi.	Anafafanua maana na aina ya mawasiliano na umuhimu wake kwa mwanafunzi kiziwi.	Anafafanua maana, aina ya mawasiliano na umuhimu wake kwa mwanafunzi kiziwi na kutoa mifano.	Anafafanua maana, aina ya mawasiliano na umuhimu wake kwa mwanafunzi kiziwi na kutoa mifano kwa kuhusianisha na mazingira.	6
		b) Kuainisha njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	Njia mbili za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi zimeainishwa.	Anaainisha njia moja ya mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi.	Anaainisha njia mbili za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi.	Anaainisha na kuelezea njia mbili za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi na kutoa mifano.	Anaainisha, anaelezea na kutofautisha njia mbili za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi na kutoa mifano.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kuainisha changamoto za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi (darasani, nje ya darasa, na kwenye jamii)	Changamoto za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi zimeainishwa.	Anaainisha changamoto za mawasiliano za darasani kwa mwanafunzi kiziwi.	Anaainisha changamoto za mawasiliano za darasani na nje ya darasa kwa mwanafunzi kiziwi.	Anaainisha na kuelezea changamoto za mawasiliano za darasani na nje ya darasa kwa mwanafunzi kiziwi.	Anaainisha na kuelezea changamoto za mawasiliano za darasani, nje ya darasa na kwenye jamii kwa mwanafunzi kiziwi na kutoa mifano.	
	3.2 Kutumia njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	a) Kubaini njia na alama za mawasiliano za awali (mf. nyumbani) kwa mwanafunzi kiziwi	Alama za mawasiliano za asili kwa mwanafunzi kiziwi zimebainishwa.	Anabainisha alama za asili za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi.	Anabainisha alama za asili za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi na kuzilinganisha na alama sanifu.	Anabainisha alama za asili za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi na kuzilinganisha na alama sanifu na kutofautisha.	Anabainisha alama za asili za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi na kuzilinganisha na alama sanifu na kutofautisha katika mawasiliano.	8

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kuchunguza uwezo wa utendaji wa milango ya fahamu katika kutoa na kupokea taarifa kwa mwanafunzi kiziwi	Uchunguzi wa kutambua uwezo wa utendaji wa milango ya fahamu katika kutoa na kupokea taarifa umefanyika.	Anaeleza namna ya kuchunguza uwezo wa utendaji wa milango ya fahamu katika kutoa na kupokea taarifa.	Anaeleza namna ya kuchunguza uwezo wa utendaji wa milango ya fahamu katika kutoa na kupokea taarifa kwa mtoto mmoja mmoja.	Anaeleza namna ya kuchunguza uwezo wa utendaji wa milango ya fahamu katika kutoa na kupokea taarifa kwa mtoto mmoja mmoja na kupendekeza mazoezi ya kuimarisha milango ya fahamu.	Anaeleza namna ya kuchunguza uwezo wa utendaji wa milango ya fahamu katika kutoa na kupokea taarifa kwa mtoto mmoja mmoja na kupendekeza mazoezi ya kuimarisha milango ya fahamu kulingana na uhitaji wa kila mtoto.	
		c) Kutumia njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi	Njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi zimetumika.	Anaeleza matumizi ya njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi.	Anaeleza na kufafanua matumizi ya njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi.	Anaeleza, anafafanua na kutofautisha matumizi ya njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi.	Anaelezea, anafafanua na kutofautisha matumizi ya njia za mawasiliano kwa mwanafunzi kiziwi na kutoa mifano.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	3.3 Kutumia TEHAMA katika mawasiliano kwa ufundishaji na ujifunzaji kwa mwanafunzi kiziwi	a) Kuchambua vifaa vya TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi	Vifaa vya TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi vimechambuliwa.	Anaainisha vifaa vya TEHAMA.	Anaainisha vifaa vya TEHAMA na kuviweka katika makundi kulingana na matumizi ya mahitaji ya mwanafunzi kiziwi.	Anaainisha, anavielezea na kuviweka vifaa vya TEHAMA katika makundi kulingana na matumizi ya mahitaji ya mwanafunzi kiziwi.	Anaainisha, anavielezea na kuviweka vifaa vya TEHAMA katika makundi kulingana na matumizi ya mahitaji ya mwanafunzi kiziwi na kutoa mifano.	8
		b) Kutumia vifaa vya TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi	Vifaa vya TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi vimetumika.	Anaelezea matumizi ya vifaa vya TEHAMA.	Anaelezea matumizi ya vifaa vya TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi.	Anaelezea matumizi ya vifaa vya TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi kwa kutoa mifano.	Anaelezea matumizi ya vifaa vya TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi kwa kutoa mifano na kutofautisha.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kubainisha njia za mawasiliano za TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi	Njia za mawasiliano za TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi zimebainishwa.	Anabainisha njia za mawasiliano za TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi.	Anabainisha na kuelezea njia za mawasiliano za TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi.	Anabainisha na kuelezea njia za mawasiliano za TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi na kutoa mifano.	Anabainisha na kuelezea njia za mawasiliano za TEHAMA kulingana na mahitaji ya mwanafunzi kiziwi na kutoa mifano kulingana na mazingira.	
4.0 Kutumia mbinu mbalimbali kuwezesha ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa kumuwezesha mwanafunzi kiziwi kuwasiliana	4.1 Kujenga uwezo wa kufundisha stadi ya kusoma	a) Kujenga stadi za lugha ya mazungumzo katika kubaini herufi	Stadi za lugha ya mazungumzo katika kubaini herufi zimejengwa.	Anaelezea namna ya kujenga stadi za lugha ya mazungumzo.	Anaelezea namna ya kujenga stadi za lugha ya mazungumzo katika kubaini herufi.	Anaelezea namna ya kujenga stadi za lugha ya mazungumzo katika kubaini herufi kwa mifano.	Anafafanua namna ya kujenga stadi za lugha ya mazungumzo katika kubaini herufi kwa mifano na kwa kuzingatia vijenzi vya lugha.	8

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kuunganisha herufi, silabi, maneno na sentensi katika kujifunza na kufundisha kusoma	Herufi, silabi, maneno na sentensi katika kujifunza na kufundisha kusoma zimeunganishwa.	Anaelezea namna ya kuunganisha herufi na silabi katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma.	Anaelezea namna ya kuunganisha herufi, silabi na maneno katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma.	Anaelezea namna ya kuunganisha herufi, silabi, maneno na sentensi katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma.	Anaelezea na kuunganisha herufi, silabi, maneno na kutunga sentensi zinazohusisha maisha yake ya kila siku.	
		c) Kutumia picha, kifungu linganifu cha habari na hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma kwa ufahamu na ufasaha	Picha, kifungu linganifu cha habari na hadithi vimetumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma kwa ufahamu na ufasaha.	Anaelezea namna ya kutumia picha katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma.	Anaelezea namna ya kutumia picha na kifungu linganifu cha habari katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma.	Anaelezea namna ya kutumia picha, kifungu linganifu cha habari na hadithi kwa kuzingatia alama za uandishi katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma.	Anaelezea namna ya kutumia picha, kifungu linganifu cha habari na hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma kwa kuzingatia alama za uandishi, mpangilio wa matukio na wahusika.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	4.2 Kutumia mbinu mbalimbali za kumuwezesha mwalimu tarajali kufundisha kuandika	a) Kubaini stadi za kuandika katika uumbaji wa herufi	Stadi za kuandika katika uumbaji wa herufi zimebainishwa.	Anabaini stadi za kuandika katika uumbaji wa herufi.	Anabaini na kuzieleza stadi za kuandika katika uumbaji wa herufi na kutumia mifano.	Anabaini na kuzielezea stadi za kuandika katika uumbaji wa herufi kwa mifano katika kuunda maneno.	Anabaini stadi za kuandika katika uumbaji wa herufi kwa kuelezea na kutumika mifano katika kuunda maneno na kutengeneza sentensi.	8
		b) Kufafanua namna ya kuandika kwa kueleweka, ushikamano na kwa mfuatano sahihi wa matukio (*kuzingatia kanuni za uandishi*) katika ufundishaji na ujifunzaji	Kuandika kwa kueleweka, ushikamano na kwa mfuatano sahihi wa matukio kumefafanuliwa.	Anafafanua namna ya kuandika kwa kueleweka katika ufundishaji na ujifunzaji.	Anafafanua namna ya kuandika kwa kueleweka na ushikamano katika ufundishaji na ujifunzaji.	Anafafanua namna ya kuandika kwa kueleweka, ushikamano na mfuatano sahihi wa matukio katika ufundishaji na ujifunzaji.	Anafafanua namna ya kuandika kifungu cha habari kwa kueleweka, ushikamano na mfuatano sahihi katika ufundishaji na ujifunzaji.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kufafanua namna ya kuandika kwa mwandiko wa chapa wenye vikonyo katika ufundishaji na ujifunzaji	Kuandika mwandiko wa chapa wenye vikonyo katika ufundishaji na ujifunzaji umefafanuliwa.	Anafafanua namna ya kuandika mwandiko wa chapa wenye vikonyo katika ufundishaji na ujifunzaji.	Anafafanua namna ya kuandika mwandiko wa chapa wenye vikonyo na kutoa mifano katika ufundishaji na ujifunzaji.	Anafafanua namna ya kuandika mwandiko wa chapa wenye vikonyo kwa kutoa mifano na kutunga sentensi katika ufundishaji na ujifunzaji.	Anafafanua namna ya kuandika mwandiko wa chapa wenye vikonyo kwa kutunga sentensi na mifano katika kuandika kifungu cha habari katika ufundishaji na ujifunzaji.	
	4.3 Kujenga uwezo wa kuchakata mbinu mbalimbali za kufundishia stadi ya kuhesabu	a) Kubaini mbinu mbalimbali za kuhusianisha vitu halisi na namba	Mbinu nne mbalimbali za kuhusianisha vitu halisi na namba zimebainishwa.	Anabainisha mbinu moja ya kuhusianisha vitu halisi na namba.	Anabainisha mbinu mbili za kuhusianisha vitu halisi na namba kwa kukusanya na kupanga.	Anabainisha mbinu tatu za kuhusianisha vitu halisi na namba kwa kukusanya, kupanga na kuorodhesha vitu halisi.	Anabainisha mbinu nne za kuhusianisha vitu halisi na namba kwa kukusanya, kupanga, kuorodhesha vitu halisi na kuzisoma.	8

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kuelezea matendo ya kuongeza na kupunguza katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuhesabu	Matendo ya kuongeza na kupunguza katika ufundishaji na ujifunzaji yameelezewa.	Anaelezea tendo la kuongeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuhesabu.	Anaelezea matendo ya kuongeza na kupunguza katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuhesabu.	Anaelezea matendo ya kuongeza na kupunguza na kutoa mifano kwa kutumia vitu halisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuhesabu na kutoa mifano.	Anaelezea matendo ya kuongeza na kupunguza na kutoa mifano kwa kutumia vitu halisi na kuhusianisha na mazingira katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuhesabu na kutoa mifano.	
		c) Kubaini vitu vinavyopimwa na kutaja vipimo rasmi na visivyo rasmi: mfano urefu, uzito na ujazo katika ufundishaji na ujifunzaji	Vitu vinavyopimwa na vipimo katika ufundishaji na ujifunzaji vimebainishwa.	Anabaini vitu viwili vinavyopimwa kwa vipimio visivyo rasmi.	Anabaini vitu viwili vinavyopimwa kwa vipimio visivyo rasmi na vipimo rasmi.	Anabaini vitu vitatu vinavyopimwa kwa uzito na vitatu vinavyopimwa kwa ujazo kwa kutumia vipimo rasmi na visivyo rasmi.	Anabaini vitu vitano vinavyopimwa kwa urefu, ufupi, uzito na ujazo kwa kutumia vipimo rasmi na visivyo rasmi katika ufundishaji na ujifunzaji na kutoa mifano.	

Orodha ya Machapisho

Brentari, D. (2016). 'The phonology of sign languages'. In *sign language and linguistics. Sandler*, United States of America: Cambridge University Press.

Emmorey, K. (2003). *Perspectives on classifier constructions in sign languages*. London, United Kingdoms: Lawrence Erlbaum Associates.

Kyle, J., Woll, B., Pullen, G., & Maddix, F. (1985). *Sign language: The study of deaf people and their language*. Cambridge, United Kingdoms: Cambridge University Press.

Lane, H. (1984). *When the mind hears*: *A history of the deaf*. New York, United States of America: Random House.

Tanzania Institute of Education. (2003). *Visual impairement syllabus for teacher education*. Dar es Salaam, Tanzania: Ministry of Education and Culture.

Tanzania Institute of Education. (2012). *Syllabus of certificate in special needs education braille skills: Mathematic notation*. Dar es Salaam, Tanzania: Ministry of Education and Vocational Training.

Tanzania Institute of Education. (2012). *Syllabus of certificate in special needs education braille skills language.* Dar es Salaam, Tanzania: Ministry of Education and Vocational Training.

Muzale, H. R. T. (2004). *Kamusi ya lugha ya alama (Toleo la pili). Languages of Tanzania Project*. Dar es Salaam, Tanzania: Dar es Salaam University Press.

Punani, B., & Rawal, N. (2000). *Handbook on visual impairment*. *The Blind People's Association*. Vasrtrapur, India: Ahmedabad.

Royal National Institute for the Blind. (1992). *Braille primer with exercises based on british braille*. (Rev.). Bakewell, United Kingdoms: Peterborough.

Valli, C., & Lucas, C. (2001). *Linguistics of American sign language. An introduction* (3rd ed.). Washington, United States of America: Clerc Books and Gallaudet University Press.